SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.20 NO. 1 2021
DOI: 10.51984/JOHS.V20I1.1583

جامعة سبها للعلوم الإنسانية مجلة
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: https://sebhau.edu.ly/journal/index.php/johs

# Matumizi ya Lugha katika Tamthiliya ya ( Sadaka ya John Okello )

Husin Hamed Husin Awhida

Department of Languages and African Studies, Faculty of Arts, Sebha University, Libya

**Keywords:**
Matumizi Ya Lugha
Kazi za Sanaa
pande za ufundi
Tamthilia
John Okello

**ABSTRACT**

Kipengele hiki hakipatikani katika lugha zote (bonyeza chache tu). Grafu iliyotangulia Ni ngapi huduma hii haipatikani katika lugha zote. Chini ni orodha ya kurasa zetu maarufu za Amerika (2015). Mazungumzo na maneno ya wimbo wa Kiingereza na tafsiri ya Kiingereza. Dunha ni mchezo wa kuigiza kuhusu mapinduzi ya serikali ya Zanzibar, ambayo yalifanyika mnamo 1964 Ambapo mtafiti alitegemea kuchanganua matumizi ya lugha katika kazi hii ya fasihi.Fasihi ni tawi la sanaa ambalo hutumia lugha ya mazungumzo au maandishi kutoa ujumbe kwa jamii. Ili ujumbe lengwa ufikie jamii, ni wazo nzuri kwa waandishi kutumia lugha kwa njia ya ubunifu katika kufikisha ujumbe kwa hadhira. Emmanuel Mbogo aliyeko Tanzania Bara, tamthiliya hiyo inawahusu watu wa Zanzibar (Ununguja na Pemba). Maneno yaliyotolewa kwa wahusika wote katika kazi hii yanahusiana na asilimia kubwa ya wenyeji wa visiwa Wahusika wote wamepewa lugha inayofaa jukumu lao. Vitu vyote vilivyotumiwa vilitoa nia tofauti, lakini kwa bahati mbaya mtafiti hakuzitumia. Vipengele vya lugha iliyotumiwa vilikusudiwa kuonyesha mada tofauti katika tamthiliya hii. Hakika misingi ya nadharia ya kimuundo kuhusu matumizi ya lugha katika kazi ya fasihi imezingatiwa katika tamthiliya hii

# الاستخدامات اللغوية فى تمثلية (صدقة جوهان أوكيلو)

حسين حامد حسين أوحيدة

قسم اللغات الأفريقية، كلية الآداب، جامعة سبها، ليبيا

**الكلمات المفتاحية:**
الإستخدامات اللغوية
الأعمال الأدبية
الجوانب الفنية
دراما
جون أوكيلو

**الملخص**

هذا المقال يبحث فى الإستحدامات اللغوية فى تمثيلية (صدقة جوهان أوكيلو) . الأجزاء المستخدمة فى اللغة تجمع كل المحتويات الأساسية التي تستخدم في الأعمال الأدبية.حيث يعد استخدام اللغة أحد الجوانب الفنية للعمل الأدبي، ويحتوى الفن على جميع المكونات الأساسية المستخدمة لإنشاء عمل أدبي على سبيل المثال الموضوعات والشخصيات والبنية والأسلوب والعنوان، وفي جانب استخدام اللغة ينظر النقاد إلى هذه الميزات؛ العبارات والاستعارات واللغات الأجنبية وما إلى ذلك حسب غرض الناقد. نستكشف في هذه المقالة استخدام اللغة في دراما التضحية للمخرج جون أوكيلو (2015). المسرحية من تأليف الكاتب التنزاني إيمانويل مبوجو. إنها دراما عن ثورة حكومة زنجبار، التي حدثت في عام 1964.حيث اعتمد الباحث على تحليل استخدام اللغة في هذا العمل الأدبي. والأدب هو فرع من فروع الفن يستخدم لغة المحادثة أو النص لإيصال رسالة إلى المجتمع. من أجل وصول الرسالة المستهدفة إلى المجتمع، من الجيد أن يستخدم المؤلفون اللغة بطريقة إبداعية في نقل الرسالة إلى الجمهور. إيمانويل مبوغو مقيم في تنزانيا القارية، دراما تدور حول شعب زنجبار (أونغوجا وبيمبا). تتوافق التعبيرات المعطاة لجميع الشخصيات في هذا العمل مع النسبة المئوية الكبيرة لسكان الجزر. يتم تخصيص لغة لجميع الشخصيات لتناسب دورهم. جميع العناصر المستخدمة قد أثارت نوايا مختلفة، لكن الباحث لم يستخدمها للأسف. هدفت عناصر اللغة المستخدمة إلى تصور الموضوعات المختلفة في هذه الدراما. بالتأكيد تم النظر في أسس النظرية البنيوية فيما يتعلق باستخدام اللغة في العمل الأدبي في هذه الدراما.

*Corresponding author:
E-mail addresses: Hus.Awhida@sebhau.edu.ly

*Article History : Received 12 March 2021 - Received in revised form 20 June 2021 - Accepted 30 June 2021*

**Utangulizi**

Matumizi ya lugha ni kipengele kimojawapo katika umbo la nje la kazi ya fasihi, yaani fani. Fani hujumbuisha viungo msingi vyote vinavyotumika kuumba kazi ya fasihi kwa mfano mandhari, wahusika, muundo, mtindo, jina la kazi/diwani n.k. Katika kipengele cha matumizi ya lugha wahakiki hutazama vipengele hivi; semi, tamathali za semi, rejesta, lugha za kigeni n.k kutegemea na lengo la mhakiki. Katika makala haya tunatalii matumizi ya lugha katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* (2015). Tamthiliya hii imeandikwa na Emmanuel Mbogo, mwanafasihi kutoka nchini Tanzania. Ni tamthiliya inayozungumzia mapinduzi ya Serikali ya Zanzibar, yaliyofanyika mwaka 1964. Nadharia ya Umaumbo ndiyo itakayoongoza mjadala wetu. Nadharia hii imeegema zaidi kwenye kuchambua matumizi ya lugha katika kazi za fasihi. Washadidi wa nadharia hii wanaona kwamba kila kazi ya kifasihi inatumia nadharia hii kwani inahusika na kipengele msingi katika tawi hili la sanaa, fasihi nguzo msingi yake ni lugha. Katika tamthiliya hii tutabainisha vipengele mbalimbali vya matumizi ya lugha huku tukiongozwa na nadharia ya umaumbo.

**1.1 Nadharia ya Umaumbo**

Nadharia ya umaumbo ni miongoni mwa nadharia zinazohakiki na kufafanua matumizi ya lugha katika taaluma ya fasihi na isimu. Nadharia hii ilitokana na wanaharakati wa pande mbili za kisomi huko Urusi: upande wa kwanza ni ule wa wanaisimu wa Moscow (Moscow Linguistics Circle) na upande wa pili ni ule wa chama cha uhakiki wa lugha ya Kishairi (Society for the Study of Poetic Language-OPAYAZ) wote wakiwa na lengo la kuleta mapinduzi kwenye isimu na uhakiki wa fasihi (Schmitz, 2007).

Wengi wa wanaharakati hawa walikuwa vijana waliojuana na kufahamiana kwani waliweza kujadiliana kwa pamoja huku wakikubaliana na kupingana kwa baadhi ya maarifa. Walikuwa na hamasa na mwamko wa kuanzisha maarifa ya kitaaluma kwa namna yoyote ile ikiwemo kwa njia ya mijadala. Katika mijadala yao walijitambulisha kama wanaurasimu (formalistics) wenye lengo la kuleta mapinduzi katika taaluma. Pia waliweza kufanya maandamano kwenye miji ya St.Peterburg na Moscow kabla ya mapinduzi ya mwaka 1917. Kutokana na juhudi za wanaharakati hawa waliweza kufunua mambo mbalimbali ya kitamaduni yaliyoko Urusi kama vile muziki, sanaa, fasihi na isimu. Kipindi cha machafuko na vita vya wenyewe kwa wenyewe wanaurasimu walipiga hatua za kudai haki zao lakini walizuiliwa na wanaukomunisti kwa kudai kwamba wanaenda kinyume na itikadi za uhalisia wa kijamaa. Walijitahidi kueleza itikadi zao lakini hawakufanikiwa na mwaka 1930 ikawa ndiyo usambalatisho wa kikundi cha wanaurasimu huko Urusi. Pamoja na msambalatisho huo mawazo yao yaliendelezwa na baadhi ya wanaurasimu kama Victor Shklovsky, Roman Jakobson na wengineo katika uwanja wa taaluma ya fasihi kwa wanataaluma wengine nje ya Urusi.

Wanamaumbo waliibua dhana kuu mbili katika fasihi: dhana ya kwanza ni ile ya uzoeaji (habitualization) na dhana ya pili ni ya ugeni (defamiliarisation). Kwa mujibu wa Carter (2006) anaona kwamba dhana ya uzoeaji inajitokeza pale jambo linapotumika mara kwa mara hadi kufikia hali ya kujiendesha lenyewe (automatically). Katika fasihi hali ya uzoeaji inaweza kujitokeza kama msomaji au msikilizaji ataiona kazi ya fasihi ni ya kawaida na akashindwa kutofautisha na kazi ya kawaida (ambayo sio ya kifasihi). Hii inatokana na kuisikia au kuisoma kazi hiyo mara kwa mara. Kutokana na dhana hii ya uzoeaji ndipo Shklovsky akatoa dhana nyingine ya ugeni au upya wa kazi za fasihi katika makala yake ya "Art as Technique" na kusema ili mwanafasihi aweze kuwasilisha hisia zake ipasavyo katika fasihi ni lazima hisia hizo azijenge katika hali ya ugeni kwa wasomaji au wasikilizaji kwa kutumia vipengele vya matumizi ya lugha (Schmitz, 2007; Carter, 2006).

Vipengele vya matumizi ya lugha ni kama vile semi, tamathali za semi, taswira, lugha ngeni au za asili zilizo tofauti na kazi yenyewe ya fasihi. Anaongezea kwa kusema ugeni wa kipindi fulani ni tofauti na ugeni wa kipindi kingine. Hii ina maana kwamba ugeni katika kazi za fasihi ni lazima ubadilikebadilike kutokana na hadhira, mada, mazingira, na wakati ambapo itaiepusha kazi ya fasihi kuwa ya kimazoea na badala yake kuipa uhai upya kila iitwapo leo. Shklovisky anasisitiza dhana ya ugeni kwa kusema sio ya kubadilisha maana bali ni ya jinsi au namna ya kuelezea jambo.

Schmitz (2007) na Carter (2006) wameainisha mawazo kadha wa kadha ya wananadharia wa umaumbo kama ifuatavyo; Kutofautisha matumizi ya lugha ya kawaida na lugha ya kifasihi, waliamini na kusisitiza kwamba dhana ya ugeni au upya ndiyo dhima kuu ya sanaa na walipenda uhakiki wa fasihi uwe na mwelekeo wa kisayansi na hivyo walitaka kuanzisha usayansi katika fasihi

Kwa mujibu wa mawazo ya wanamaumbo, kazi zote za fasihi hutumia nadharia hii kwa sababu kazi ya fasihi haiwezi kuwa ya kifasihi kama haitakuwa na usanaa ndani yake. Sanaa hizo ni ujenzi wa vipengele vya lugha vinavyoonesha upya wa kazi hiyo. Hivyo basi mtu yeyote atakayehakiki kazi yoyote ya fasihi kwa kuzingatia nadharia ya umaumbo ni wazi swala la "upya" yaani vipengele vijengavyo matumizi ya lugha haviwezi kuepukika.

Kwa kuhitimisha nadharia ya umaumbo imechangia kwa kiasi kikubwa harakati za ukuzaji na maendeleo ya uhakiki wa fasihi. Mchango huo umetokana na dhana ya ugeni au upya katika kazi za fasihi, changamoto na mijadala mbalimbali iliyoibua maarifa na mawazo mbalimbali katika taaluma ya fasihi na uanzishaji wa nadharia nyingine kama ile ya nadharia ya usasa.

**1.2 Matumizi ya Lugha katika Tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello***

**1.2.1 Tashbiha**

Hii ni tamathali ya semi inayounganisha vitu viwili au zaidi vyenye mshabaha. Maneno yanayotumiwa zaidi katika tamathali hii ni haya; kama, mithili ya, mfano wa, kama vile, n.k Katika tamthiliya yetu teule tamathali hii imejitokeza pahala pengi. Mtunzi wetu Emmanuel Mbogo amejitahidi kuitumia kila onyesho kadri ya masemezano ya wahusika wake. Tashbiha zilizojitokeza ni hizi zifuatazo:

"…Uhuru wa Zanzibar unanukia **kama** marashi ya Pemba…" (uk.1)

"***Kama*** nahodha wa meli!" (uk.4)

"***Kama*** rubani wa ndege!"(uk.4)

"***Kama*** jemedari wa jeshi"(uk.4)

Katika kauli walizopewa wahusika hawa, tashbiha ***"kama"*** imejitokeza. Sehemu ya kwanza uhuru wa Zanzibar unalinganishwa na marashi ya Pemba. Hapana shaka wazawa wa Zanzibar waliusubiri kwa hamu kubwa sana uhuru kutoka kwa wakoloni, hata dalili ilipoanza kuonekana kwamba wataupata wakaufananisha na marashi ya Pemba, yanayoonekana kivutio kwa wakazi hao wa

Kisiwani Unguja. Pia katika uk. 4 mtunzi amemfananisha Sultan Jamshid na vitu mbalimbali kama vile nahodha, rubani na jemedari. Neno ***kama*** limetumika kufanya ulinganisho huu katika tamthiliya hii ya *Sadaka ya John Okello*.

**1.2.2 Tashihisi**

Hii ni tamathali inayotumika kwa kuvipa viumbe sifa za kutenda kama binadamu, kwamba kitu kisicho na uhai kupewa uwezo wa kufanya kama mwanadamu afanyavyo. Katika ukurasa wa sita ndani ya tamthiliya teule, Mhusika RASHID ametumika kuonyesha tamathali hii ya tashihisi. Rashid anasema,

"Ati sina mama, ***mbuyu*** ulipasuka, nikazaliwa?" (Uk.6)

Mbuyu ni mmea. Jinsi mimea inavyozaana ni tofauti na binadamu anavyozaliwa. Kwenye tamko hili la RASHID mmea huu umepewa sifa ya kuzaa kama binadamu. Tashihisi hii imetumika kuibua tafakuri kwa wakoloni waliokuwa wakiwatesa wakazi wa Zanzibar, kwamba wawaheshimu hawa watu weusi pia ambao wamezaliwa kama binadamu wengine.

Vilevile katika uk.3 mtunzi anasema, "***Historia iliyofumbata ua la Alizeti au ua la Waridi."*** Uwezo wa kushika kitu na kufumbata anao binadamu. Binadamu hufumbata kitu kupitia mikono yake. Katika kauli hii mtunzi anaipa historia uwezo wa kibinadamu, kwamba hushikilia, hutunza na kuhifadhi mambo mazuri zaidi. Maua ya Alzeti na Waridi yametumika kuakisi mambo mema, mazuri yanayovutia katika jamii.

**1.2.3 Kejeli au Kinaya**

Katika tamathali hii maneno yanayotolewa huwa na maana tofauti kabisa na maana lengwa. Inamhitaji hadhira kuwaza kwa kina ili kung'amua maana inayorejelewa. Mtunzi ametumia tamathali hii pia katika tamthiliya hii teule. Kwa mfano,

**OKELLO**: *...wote watatu wana kasi ya kobe…*(uk.10)

Watu hawa watatu wanaosemwa humo na mhusika Okello kasi yao ya utendaji imeshushwa mno. Imepunguzwa mno hata kufikia kulinganishwa na mwendo wa kobe ambao wajulikana kuwa taratibu mno, kwa lugha isiyoweza kutamkika. Hakika hii ni kejeli au kinaya kwa walengwa katika kauli hii. Wanakumbushwa kufanya mambo kwa wepesi zaidi.

**1.2.4 Dhihaka**

Hii ni tamathali yenye ubeuzi mkali sana (Senkoro 1981). Maneno yanayosikika ni tofauti na maana lengwa kabisa. Mhusika mmoja, BIBI ametumiwa na mtunzi kuwakilisha tamathali hii ndani ya tamthiliya teule.

BIBI: **…***Mungu mnayemwabudu amekuwa mjomba wenu?...*(uk.64)

Mhusika BIBI anauliza swali kwa watu wanaoonekana kumwabudu Mungu kila uchao huku matendo yao yamejaa dhuluma na uonevu mkali. Matendo wanayoyafanya haya akisi mafunzo ya Mwenyezi Mungu. Wanatesa watu, watumwa na wengine wote wanaokatiza mbele ya macho yao wasio na rangi kama yao. Swali hili hakika ni dhihaka kwa hao wanaoonekana kumcha Mungu huku wakitenda maovu. Mtunzi anasema, Mola hachezewi, hadanganywi, hafanyiwi dhihaka kama ambavyo mwanadamu anaweza kufanya kwa mjomba wake.

**1.2.5 Takriri/Shada**

Haya ni maneno yanayotolewa kusisitiza au kutilia mkazo jambo fulani. Mbinu hii inajitokeza zaidi katika utanzu wa ushairi ingawa katika tanzu nyingine hujitokeza pia (Mulokozi 1999). Takriri inaweza kujitokeza kwa kurudiwa rudiwa neno au mizani au mkarara au kina. Katika tamthiliya teule, *Sadaka ya John Okello* tamthali hii imetumika. Mtunzi ametumia takriri hizi;

ASHURA: *"Leo! Leo!" Leo saa ngapi…* (uk.14)

Takriri imejitokeza kama neno '*leo*' katika tamko hilo la mhusika Ashura. Mhusika huyu ametumika neno hili kuonyesha msisitizo. Anataka mwenzake abainishe waziwazi hilo analolisema atalikamilisha leo saa ngapi? Maana siku ya leo ina masaa mengi.

**1.2.6 Semi**

Mulokozi (1996) anasema semi ni kauli fupi zilizobeba maana nzito ndani yake. Katika fasihi simulizi ya Kiswahili inadaiwa kuwa semi ni tokeo la idili ndefu za kimaisha walizopitia wahenga, ndiyo maana mara nyingi zinaonekana kuwa kweli kila zinapotolewa. Katika utanzu huu kuna vipera mbalimbali mathalani, methali, vitendawili, nahau na misemo.

Methali zimetumika katika tamthiliya hii teule. Aina hii ya semi huwa na pande mbili, upande wa kwanza hueleza jambo na upande wa pili hueleza tokeo lake. Emmanuel Mbogo ametumia methali hizi;

RAMADHANI**: …***Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu* (Uk.10)

OKELLO: *Chenye mwanzo, kina mwisho* (uk.17)

RASHIDI:…*Ni dua tu la kuku lisilomtisha mwewe*…(uk.17)

OKELLO***: Shukrani za punda, mateke.*** (uk.67)

*Mvumilivu, hula mbovu* (uk.68)

Methali hii ya *Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu* hutumika kuhamasisha umoja miongoni mwa wanajumuiya. Huweka msisitizo watu kushikamana pamoja katika jambo lolote wanaloliendea. Methali hii ameitumia mtunzi kupitia muhusika waje Okello alipokuwa akiwahamasisha vijana wenzake kuingia vitani ili kufanya mapinduzi na hatmaye kujipatia uhuru wa kweli katika ardhi yao. Methali mbili za mwisho; Shukrani ya punda, mateke na mvumilivu hula mbovu ni tokeo la majuto anayopitia mhusika wa tamthiliya hii teule, John Okello. Mhusika mkuu huyu amechangia pakubwa katika ukombozi wa nchi mbalimbali hapa Afrika (Zanzibar ikiwepo) lakini hakukumbukwa pahala popote. Kila alipokamilisha ukombozi alifukuzwa na kuishia gerezani. Mtunzi ametumbia mbinu ya udenguzi, kusema methali kwa kinyume badala ya kusema mvumilivu hula mbivu akaandika, mvumilivu hula mbovu. Hii yote ilikuwa kuonesha sikitiko la mhusika huyu Okello.

**1.2.7 Misemo**

Hizi ni kauli fupifupi ambazo hutumiwa na jamii kusisitiza ukweli wa jambo fulani. Inasemwa kwamba kauli hizi huunganisha dhana au mawazo tofauti kuwa jambo moja kwa lengo la kufikisha ujumbe uliodhamiriwa. Ndani ya tamthiliya teule, *Sadaka ya John Okello* mtunzi ametumia misemo mbalimbali. Kwa mfano;

OKELLO: *Mfungwa hachagui jela* (uk.67)

OKELLO: *Mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni***.** (uk.68)

Methali hizi zimetoka katika kinywa cha mhusika mkuu wa tamthiliya hii teule. Ni hakika kuwa mfungwa huwa hachagui jela ya kuwekwa, wanaoamua hatma yake ni mabwana zake waliomuhukumu. Anasikitika Okello kwa uovu aliofanywa, amefanya jitihada kubwa lakini ameishia jela, tena mbali na alikofanyia mapinduzi! Mtunzi anaendelea kuiambia jamii kwamba watu wanyonge wasionewe bali wapewe haki zao.

**1.2.8 Lugha ya Kigeni**

Ndani ya tamthiliya teule imetumika pia lugha ya kigeni, kiingereza. Mtunzi ametumia lugha hii ili kuakisi upya unaosemwa na wanamaumbo, kazi ionekane mpya na ujumbe ufike sawasawa kwa hadhira yake. Katika ukurasa ya 17 kuna neno limetoholewa *"Kumobilaizi"*. Katika lugha ya Kiingereza neno hili huandikwa *'Mobilization'* likimaanisha kuunganisha nguvu pamoja. Mtunzi hapana shaka ametohoa neno hili ili kuleta upya katika kazi yake. Mhusika BABU anasema hivi;

BABU: *Tunahitaji kumobilaizi umma ili kuinua urazini wao wa kisiasa. Urazini wao ukifika*

*kileleni mintarafu nadharia ya Marxism – Leninism na ile ya Dialectical Materialism na*

*Class – Struggle ee… yaani mivutano na minyukano kati ya mabepari na wafanyakazi* (uk.17)

Lugha ya kiingereza inadhihirika kupitia kauli za muhusika huyu BABU. Mtunzi ametumia maneno hayo kutambulisha nadharia mbalimbali zilizoongoza mapambano katika jamii za Ulaya hata watu wakafikia ukombozi wa kweli. BABU anaeleza kwamba, watu wakifahamu nadharia hizo zote basi wanaweza kufanya mapinduzi hayo wanayotaka kuyaendea.

**1.3 Maoni na Mapendekezo**

Mtunzi wetu, Emmanuel Mbogo ametumia vizuri sana lugha katika ujenzi wa tamthiliya hii. Kuanzia mwanzo hadi mwisho msomaji hakinai kuiendea kazi hii. Upya unaosemwa na wanamaumbo katika nadharia hakika unajitokeza katika kazi hii. Kwa vile lugha imetumika vema basi hata ujumbe uliokusudiwa kuifikia hadhira bila shaka utafika. Ujuzi huu auendeleze.

**1.4 Hitimisho**

Fasihi ni tawi la sanaa linalotumia lugha ya mazungumzo au maandishi kufikisha ujumbe kwa jamii. Ili ujumbe lengwa uweze kufika kwa jamii ni vema watunzi wakatumia lugha kiubunifu katika kuifikishia hadhira ujumbe huo. Emmanuel Mbogo ni mkazi wa Tanzania bara, tamthiliya aliyoitunga inahusu watu wa Zanzibar (Unguja na Pemba). Matamshi waliyopewa wahusika wote katika kazi hii yanaendana na wakazi wa visiwani asilimia kubwa. Alipoongea mwarabu, lugha imemtambulisha. Alipoongea mzawa wa Unguja, lugha imemtambulisha, alipoongea mtumwa kutoka bara, kwenye msafara wa watumwa kutoka Tabora naye lugha imemtambulisha. Wahusika wote wamepewa lugha kuendana na uhusika wao. Vipengele vyote vilivyotumika vimeibua dhamira mbalimbali, mtunzi hakuvitumia kwa bahati mbaya. Vipengele hivi vya lugha vilivyotumika vililenga kuibua dhamira mbalimbali ndani ya tamthiliya hii. Kwa hakika misingi ya nadharia ya umaumbo kuhusu utumizi wa lugha katika kazi ya fasihi imezingatiwa ndani ya tamthiliya hii.

**Marejeo**

[1]- Carter, D. (2006). *Literary Theory*. Pocket Essentials: Herts.

[2]- Kobia, (2008). "*Nadharia ya Utendaji Katika Uhakiki wa Fasihi ya Kiafrika: Nyimbo za Tohara za Walgembe wa Meru Kaskazini kwenye*" Kitabu cha Nadharia Katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika. Moi University Press: Eldoret.u

[3]- Odeo, I. I. (2008). "*Nafasi ya Nadharia Katika Ufundishaji wa Kiswahili Katika Shule na Vyuo*" kwenye Kitabu cha Nadharia Katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika. Moi University Press: Eldoret.

[4]- Said, A.M.K (2008). "*Nadharia, Ubunifu, Uchambuzi na Taaluma ya Kiswahili*" Kitabu cha Nadharia Katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika. Moi University Press: Eldoret.

[5]- Schmitz, T. A (2007). *Modern Literary Theory and Ancient Texts: An Introduction*. Blackwell Publishing Ltd: Carlton.

[6]- Tilak, R. (1993). *History and Principles of Literary Criticism*. Rama Brothers: New Delhi

[7]- Mulokozi, M.M. (1996), *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*, Dar es Salaam: TUKI.

[8]- Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha*. Dar es Salaam: Education Publishers and Distributor, Ltd.

[9]- Msokile, M. (1993). *Miongozo ya Lugha na Fasihi: Uchambuzi na Uhakiki wa Riwaya*, Dar es Salaam: DUP.

[10]- Mwaifuge, E. S. (2006), "Fasihi ya Kiswahili na Rushwa Tanzania: Thomas A. R. Kamugisha na Kitu Kidogo Tu," katika, Kioo cha Lugha, Juzuu namba, 4, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 39-45.

[11]- Nazarova, T. (1996), Linguistics and Literary Semiotics, Moscow: Moscow State University Press.

[12]- Ndungo, C. (1991), Misingi na Nadharia ya fasihi ya Kiswahili.Nairobi:JKF. Njogu, K.

[13]- Rocha, C. (1999). Ufudishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu. Nairobi: JKF.